# BE READY.
# STAY COVERED.

## Maulizo yanayoulizwa sana kuhusu Kufanya Mpya Medicaid

*Imefanywa mpya Septembea 2023*

**Kufanya mpya Medicaid ni nini?**

Mbele ya COVID-19, serikali iliangalia tena kila mwaka habari ya wanamemba ya Medicaid kwa kuhakikisha wanastahili. Hatua hii imeitwa “Kufanya mpya.”

Serikali ya jimbo ilisimamisha kufanya mpya kwa wakati ya COVID-19 kwa kuhakikisha watu walichunga bima yao ya afya. Wakati msaada ya haraka ya jamii ilipoisha, serikali ya jimbo iliomba majimbo kuanza kufanya mpya tena.

Rhode Island ilianza kufanya mpya tena Medicaid kwa mwezi wa ine 2023. Tangu hapo zaidi ya wanainchi ya Rhode 350,000 waliandikishwa kwa Medicaid, si kila mutu atafanywa mpya mara moja. Habari za kufanya mpya itatolewa kwa watu mbalimbali kwa mwanzo ya kila mwezi. Inamaanisha ya kwamba wanamemba watapata habari kwa barua kutoka serikali mara ingine kati ya sasa na mwezi ya ine 2024

Kama majimbo mengine, Rhode Island ilichelewesha shughuli ya kusajiliwa upya kwa familia zilizo na watoto ili kutoa muda zaidi wa ushiriki na mawasiliano ya busara. Ikiwa mtoto au watoto katika familia yako wamesajiliwa katika Medicaid, utapokea notisi kati ya Desemba 2023 na Aprili 2024.

**Je, kila mtu katika familia yangu atasajiliwa mara moja?**

Ndiyo, washiriki wa Medicaid wanaoishi katika familia moja watasasishwa pamoja. Wanafamilia wote wataorodheshwa kwenye notisi moja. Hata hivyo, ustahiki wa wanafamilia tofauti unaweza kukaguliwa kwa njia tofauti.

Kwa mfano, Serikali inaweza kuhitaji taarifa zaidi kuhusu mtu mzima katika familia na kuomba hati. Lakini Serikali inaweza pia kuwa na maelezo ya kutosha kuhusu mtoto aliye chini ya umri wa miaka 19 katika familia ili kusajili upya huduma ya mtoto kiotomatiki.

**Nitafanya nini kwa kujitayarisha?**

Kuna maneno tatu unawezafanya kwa kukuwa tayari na kubaki kwa bima.

1. **Fanya mpya njia ya habari yako.** Hakikisha serikali ina anwani yako ya sasa, namba ya simu na email.
2. **Angalia kwa habari ya rangi ya manjano ao majani katika barua.** Serikali inawezakukuambia kama bima yako inajifanya mpya yeye mwenyewe ao itakuuliza kutoa habari zaidi.
3. **Chukua hatua mara moja.** Tafazali tuma ile fomu yako umeweka sahihi na mabarua zingine zote zile serikali alizoziomba kwa haraka. Unapasha kutuma barua yako kwa ile tarehe uliyopewa.

**Nitafanya mpya njia yangu ya kupata habari namna gani?**

Unaweza kufanya mpya njia yako ya kupata habari kwa namna mbalimbali:

- **Kwa mtandao ao kwa njia ya simu**: Tembeleahealthyrhode.ri.gov kwa kutupata kwa mtandao ao pakua HealthyRhode kwa simu yako kwa kufikia akaunti yako. HealthSource RI (HSRI) pya inakaribisha mazungumuzo kwa mtandao wakati ya masaa ya kazi kwa healthsourceri.com.
    - Wanamemba wote wa Medicaid wana akaunti ile iliundwa wakati ulipokubaliwa kwa Medicaid. Ikiwa bado unatengeneza akaunti yako kwa mara ya kwanza, unaweza kuingiza namba yako ya ulinzi ya kijamii na siku ya kuzaliwa kwa kupata jina yako ya kutumia. Halafu fuata hatua kwa kuweka mpya neno ya siri.
- **Zungumuza na shirika inayosimamia bima yako ya afya**: Uko na kadi yeyote ya bima kutoka kwa Neighborhood Health Plan of Rhode Island, Tufts Health Plan (RITogether) ama United Health Care Community Plan (UHCCP)? Ita namba inayopatikana nyuma ya kadi yako kwa kusaidia kufanya mpya njia yako ya kupata Habari.
- **Kupitia simu**: Ita HSRI at 1-855-840-4774 (Siku ya kwanza hadi siku ya tano, ila tu siku ya pumuziko, tangu 8 a.m. hadi 6 p.m).
- **Kwa binafsi**: Wafanya kazi kwa ofisi ya Rhode Island ya kusimamimia wafanya kazi (DHS) wanaweza kusaidia wateja kwa binafsi. Kwa orodha ya ofisi za DHS, tembelea dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices.

**Wakati yangu ya kufanya mpya itakuwa gani?**

Kwa kupata mbele tarehe yako ya kufanya mpya Medicaid yako, ingia kwa akaunti yako kwa healthyrhode.ri.gov na utafute “Habari yangi ya kufanya mpya.”

Serikali itakutumia pya habari miezi mbili mbele uhitaji kutimiza kufanya mpya bima yako. Kwa mufano, ikiwa kufanya mpya yako itahitajika kutimizwa kwa mwisho ya mwezi wa tano kwa kuchunga faida yako kuanza kwa mwezi wa sita, utapata habari ya kufanya mpya kwa mwezi wa ine. Habari itakujulisha kama Medicaid yako itafanywa mpya yeye yenyewe ao kama unahitaji habari zaidi kuhusu jamaa yako kwa serikali. Habari itakujulisha pya tarehe ya mwisho kwa kurudisha fungu ya kufanya mpya ile uliweka sahihi.

**Namna gani sijapata habari katika barua kuhusu kufanya mpya bima ya Medicaid?**

Wote wale Medicaid yao itakubaliwa kuangaliwa tena na serikali wangepata barua ya mwanzo ya kufanya mpya Medicaid yao kwa mwezi wa tatu. Barua hii ilikuambia kuhusu hatua ya kufanya mpya Medicaid na namna gani ni ya maana kuwa na uhakika tuko na njia ya kamili kwa kukutumia habari.

Kama haukupata hii barua kwa sanduku yako ya barua ao kwa akaunti yako kwa healthyrhode.ri.gov, tafazali angalia njia ya kukutumia babari mara moja.

Serikali itakutumia habari zingine kwa barua wakati ni muda yako kwa kufanya mpya bima yako.

**Nitapata usaidizi namna gani kwa kufanya mpya bima yangu?**

Usaidizi unapatikana kwa binafsi, kupitia simu na kwa mtandao. Kujua kuhusu njia hizi, tembelea staycovered.ri.gov/medicaid-renewals/contact-us.

- Watu wa kukubaliwa wako tayari kukusaidia bila malipo, kwa usaidizi ya binafsi. Mashirika mingi ya kutegemea jamii wanaweza vile kukusaidia kufahamu kufanya mpya Medicaid yako na hatua za kufuata.

- Ukiwa na miaka 60 ao zaidi ao mtu mzima na kilema, unawezaita Point, 401-462-4444. Ukiwa na mika 65 ao zaidi ao mwenye kupokea Medicaid, unawezaita call 888-884-8721. Washirika na vituo vya juu na mashirika ya kazi ya jamii wanaweza pya kusaidia.
- Kwa kupata usaidizikaribu yako, tembelea staycovered.ri.gov/community-support.

**Nitaleta barua zangu kwa serikali namna gani?**
Kama sehemu ya hatua ya kufanya mpya, serikali inaweza kukuuliza kuleta barua zingine Kuna njia mingi unaweza kufanya ile, ikiwa mtandao, kwa barua ao binafsi.

- **Kwa mtandao ao kwa njia ya simu**: Tembeleahealthyrhode.ri.gov kwa kutupata kwa mtandao ao pakua HealthyRhode kwa simu yako kwa kufikia akaunti yako.
- **Kupitia posta:** Unaweza tuma barua zilizoombwa kwa P.O. Box 8709, Cranston, RI 02920- 8787.
- **Kwa binafsi**: Wafanya kazi kwa ofisi ya Rhode Island ya kusimamimia wafanya kazi (DHS) wanaweza kusaidia wateja kwa binafsi. Kwa orodha ya ofisi za DHS, tembelea dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices. Unaweza pya kutuma barua ukitumia RI DHS Scan Center kwa 1 Reservoir Ave., Providence.

**Site ya Kufanya Upya Medicaid ni nini?What is the Medicaid Renewal Lookup Portal?**
Site mpya ya Kufanya Upya Medicaid inaweza kutumika kupata tarehe yako inayotarajiwa ya kulipia upya Medicaid. Site hii ni rahisi na salama na hakuna haja ya kuingia katika akaunti. Site hii inaweza kubadilishwa kuwa Kiingereza, Kihispania na Portugais. Kama kuna mtu anakusaidia kufanya upya, anaweza kutumia site pia. Unapasha kufanya hivi:

- Weka namba ya kitambulisho cha Medicaid iliyo kwenye kadi yako nyeupe ya Anchor.
- Weka tarehe yako ya kuzaliwa.

Site itakuambia wakati unaweza kutarajia kufanya upya. Lakini kumbuka, tarehe yako ya kufanya upya inaweza kubadilika kwa hivyo angalia tena mara nyingi.

Baada ya kujua tarehe yako inayotarajiwa ya kufanywa upya, unaweza kujitayarisha. Unapasha:

- Kufanya mpya njia ya habari yako.
- Angalia barua yako ili upate bahasha ya manjano ao majani.

**Nilikosa tarehe ya mwisho kwa fungu yangu. Nitafanya nin?**
Ikiwa ulikosa tarehe ya mwisho juu ya bahasha yako ya fungu ya kufanya mpya ya kimanjano, weka sahihi kwa fomu ya kufanya mpya na tuma barua yako mara moja.
*Kama serikali inapata fungu yako kati ya siku 90 ya tarehe faida yako ilisimama (kufuatana na Barua ya Uamuzi ya Faida), barua zako zitakubaliwa na kuchaguliwa kwako itaangaliwa tena.*

- Kama serikali inapata barua zako kati ya siku 90 na kuamua unakubaliwa kwa Medicaid, bima yako itarudishwa. Utapata kadi ya nyeupe ile unawezatumia kwa dawa na kwa kuona wanganga ikiwa wenye kutoa kazi wanakubali beyi-kwa-kazi ya Medicaid. Hapo utaandikwa tena kwa mpunggo yako ya afya ya kusimamiwa (Neighborhood Health Plan of Rhode Island, Tufts Health (RITogether) Plan, au UnitedHealthcare Community Plan (UHCCP)).
- Kama serikali itapata barua zako kati ya siku 90 na kuamua hausathili tena kwa Medicaid, unawezapewa habari kuhusu namna gani kupata bima ya afya ya beyi chini kupitia HealthSource RI. Habari ya Uamuzi ya Faida yako itatolewa pya kuhusu namna gani kutakuomba uamuzi ingine.

Kwa kujua zaidi kuhusu njia zingine ya bima yako wakati barua zako za mwisho zinapochunguzwa, ita HealthSource RI (HSRI) tangu 8 a.m. hadi 6 p.m kwa siku za juma kwa 1- 855- 840- 4774.

**Nini inatokea kama sikubaliwe tena kwa Medicaid?**
Ikiwa haukubaliwe tena kwa Medicaid, kundi muzuri ya kusaidia kwa HealthSource RI inaweza kukusaidia kupata bima muzuri ya afya.
Kulingana na ukubwa ya watu kwa nyumba na mapato yako, unawezastahili kwa:

- Kujiandikisha yenyewe kwa mupango ya afya inayojulikana (QHP)na miezi mbili ya usaidizi ya juu
- Miezi mbili ya usaidizi ya juu na kukuposha ya ushuru ya malipo ya kwanza ya jimbo
- Kukopesha ya usuhuru ya kwanza y ajimbo inafanyiza bima ya afya kuwa nepesi.

**Namna gani kuuliza uamuzi kuchungwa tena?**
Kuna njia chache ya kuomba uchunguzi kufanywa tena kulingana na bima yako ya Medicaid. Unaweza kuuliza:

- **Mtandaoni**. Ingia kwa akaunti yako kwa healthyrhode.ri.gov na finya kwa "jaza ombi".
- **Kupitia simu**. Unaweza jaza ombi kwa kuita HealthSource RI kwa 1- 855- 840- 4774.
- **Kwa binafsi**. Kwa orodha ya ofisi za DHS, tembelea dhs.ri.gov/about-us/dhs-offices. Fomu ya ombi inakuwa ndani ya kila Habari ya Uamuzi ya Faida. Jaza ile fomu na kuja nayo.
- **Kupitia posta**. Fomu ya ombi inakuwa ndani ya kila Habari ya Uamuzi ya Faida. Jaza ile fomu na kuja nayo kwa ATTN: Appeals State of Rhode Island, P.O. Box 8709, Cranston, RI 02920- 8787.

Maagizo namna gani kujaza ombi zinapatikana pya katika Habari ya Uamuzi ya Faida. Ili upate maelezo zaidi, tembelea staycovered.ri.gov/medicaid-members/file-appeal.

***Mtoto mtegemezi anayeishi katika familia yangu ameandikishwa katika Medicaid ya Rhode Island. Ninatakiwa kufanya nini ili kuwa tayari kwa ajili ya kulipia upya?***
Kuna maneno tatu unawezafanya kuhakikisha uko tayari na kubaki kwa bima.

1. **Fanya mpya njia ya habari yako.** Hakikisha Jimbo ina anwani yako ya sasa, namba ya simu, na barua pepe ili uweze kupata habari muhimu kuhusu bima yako.
2. **Angalia kwa habari ya rangi ya manjano ao majani katika barua.** Serikali inawezakukuambia kama bima yako inajifanya mpya yeye mwenyewe ao itakuuliza kutoa habari zaidi.
3. **Chukua hatua mara moja.** Tafazali tuma zile fomu zako umeweka sahihi na mabarua zingine zote zile serikali alizoziomba kwa haraka. Unapasha kutuma barua zako kwa ile tarehe uliyopewa.

***Ulipaji wangu upya utafanyika lini?***
Jamii zilizo na watoto, ambazo ni pamoja na mtu yeyote wa chini ya miaka 19, zitapata habari ya kuwajulisha wakati ukifika wa kulipia upya. Utaweza tu kuchukua hatua ya kulipa upya bima yako baada ya kuipokea baadaye. Habari hii itakuja kati ya Desemba 2023 na Aprili 2024. Habari hii itakuja kila wakati mwanzoni mwa mwezi.
Ili kutafuta tarehe yako inayotarajiwa ya kulipia Medicaid, tembelea staycovered.ri.gov na utumie Site ya Kulipia Upya Medicaid.
Pia unaweza ingia kwa akaunti yako kwa healthyrhode.ri.gov na utafute “Habari yangi ya kufanya mpya.”

***Jamii au walezi wa kisheria wanaweza kupata wapi usaidizi wa moja kwa moja wa kulipia upya?***

Tunajua kwamba wakati mwingine, ni rahisi kuongea moja kwa moja na mtu anayeweza kukusaidia kulipia upya Medicaid. Unaweza kupata usaidizi wa bure kutoka kwa mtaalamu aliyefundishwa karibu na wewe. Washauri waliothibitishwa wa kusaidia kwa maombi (CAC) na Waelekezi wako hapa kwa ajili yako. Wanakusaidia kupata habari na kufanya maamuzi kuhusu bima yako ya afya. Wataalamu hawa watakusaidia:

- Kuelewa ni nani anaweza kupata Medicaid (kukubalika)
- Kujaza fomu
- Kupata habari kuhusu bima ya Medicaid
- Kutuma malalamishi au kuwasilisha malalamishi
- Kuilinda kutokana na ulaghai
- Pata habari kuhusu chaguo zingine za bima ya afya ikiwa haukubaliki tena kwa Medicaid

Ukitaka kupata habari zaidi kuhusu usaidizi wa eneo husika, tembelea staycovered.ri.gov/community-support.

***Nini inatokea kwa bima ya mtoto wangu kama sikubaliwi tena kwa Medicaid?***
Mtoto bado anaweza kukubaliwa kupata bima ya Medicaid hata kama mzazi ao mlezi wa kisheria hakubaliwi tena. Hii ni kwa sababu kiwango yako ya mapato ya jamii kwa watoto ni kubwa kuliko ya wazazi na walezi.

Ikiwa wewe na/ao watoto ambao wanakutegemea katika jamii yako haukubaliwi tena kwa Medicaid, kundi muzuri ya kusaidia kwa HealthSource RI inaweza kukusaidia kupata bima muzuri ya afya.
Kulingana na ukubwa ya watu kwa nyumba na mapato yako, unawezastahili kwa:

- Kujiandikisha yenyewe kwa mupango ya afya inayojulikana (QHP)na miezi mbili ya usaidizi ya juu
- Miezi mbili ya usaidizi ya juu na kukuposha ya ushuru ya malipo ya kwanza ya jimbo
- Kukopesha ya usuhuru ya kwanza y ajimbo inafanyiza bima ya afya kuwa nepesi

***Kila mtu katika jamii yangu atafanyiwa upya mara moja?***
Ndio, washiriki wa Medicaid ambao wanaishi katika jamii moja watafanywa upya pamoja.

***Ninapasha kufanya kitu yoyote tofauti ili kufanya upya bima ya mtoto wangu nikifananisha na bima yangu?***
Watoto wadogo ambao wanategemea watu wengine kwa jamii yako wanaweza kufanywa upya kiotomatiki kwa kutumia njia ya kulipa ya Ripoti Mabadiliko Peke. Ikiwa kuna mabadiliko kwa hali ya mtegemezi wako, lazima utuambie. Wazazi ao walezi wachache katika jamii moja wanaweza kuhitaji kutoa fomu au habari fulani. Huu ni ulipaji upya wa Hatua Inahitajika. Aina zote mbili za ulipaji upya zitaonekana katika habari moja ya kulipa kwa familia.

**Mtoto anaweza "kuzeeka" atoke kwa Medicaid?**
Kijana anapokuwa na umri wa miaka 19, hapashi tena kuwa katika Medicaid kama mtegemezi katika jamii ya Medicaid.
Lakini anaweza kukubaliwa kupata bima ya afya:

- Kwa aina tofauti ya Medicaid
- Kupitia mpango wa bima ya HealthSource RI

***Mtoto wangu wa miaka 19 anapasha kufanya nini baadaye?***

Ukipokea habari yako ya kulipa upya ya Medicaid, itasema "Hatua Inahitajika." Fuata mashauri ambayo yamepeanwa kwa habari yako ili kuripoti mabadiliko yoyote katika hali ya jamii yako. Pia utapokea barua nyeupe inayosema, "Fomu za Ziada Zinahitajika" (tutatuma barua hii kando).

Hakikisha umesaini barua yako ya kuweka upya ya manjano. Tafadhali tutumie, pamoja na fomu zozote zinazohitajika, **kabla ya tarehe ya mwisho** kwenye ilani yako ya manjano.

***Itakuwaje ikiwa mtegemezi wangu alikuwa katika huduma ya DCYF lakini kesi yake haitumiki tena?***
Mtegemezi wako hawezi tena kuwa chini ya uangalizi wa DCYF kwa sababu:

- Amerudia jamii yake
- Amefika miaka 18

Hatapata notisi ya kulipa upya Medicaid ya manjano. Atapata barua ya majani ambayo inamjulisha kuwa hakubaliwi Medicaid.

Ikiwa anataka kubakisha Medicaid, lazima atume ombi kwa kukamilisha ombi ya DHS-2 ya usaidizi ili tuweze kuamua ikiwa anakubaliwa.

***Niko na ujauzito. Ninakubaliwa kwa Medicaid?***
Watu wajawazito wa umri wowote wanaofikisha kiwango ya mapato wanakubaliwa Medicaid wakiwa wajawazito na kwa miezi 12 baada ya kutokuwa wajawazito tena (baada ya kupata mtoto).